MAHUBIRI N°12: KANISA NA SERIKALI

(*Ilihubiriwa jumapili asubuhi 27 aprili 2003 pa Locodjro, Abidjan – Côte d'Ivoire /* www.matth25v6.org)

Je! Munaelewa kwa nini msingi wa ono ni kitabu cha Danieli? Kwa wakati wa Danieli, Nebukadneza akafanya shauri pamoja na wachawi wake wote na akasimamisha sanamu ndefu kama CNEPE-CI, ya urefu wa makanisa 600. Danieli sura 3. Na wakaldea wakamwambia mfalme: *"Watu hawa hawakujali wewe, Ee mfalme! Hawaheshimu miungu yako (makanisa) na sanamu (CNEPE-CI) uliyoifanya"...* Tangu miaka hizo kumi za mwisho, tunaona miungano kubwa kubwa na mashirikisho za makanisa katika nchi zote. Na hiyo ni utimilifu wa Mat.13:24-30. Na ujumbe huu unakuja pia kwa kukusanya wateule. Kuukataa, ni kuchagua kujitetea haki hukumuni mwa Mungu badala ya kuchagua neema. Na sasa ninapenda kutia nukta ya mwisho ya muhimu. Naamini wakati umetimia na hayo yanarudi kwa utaratibu wa kazi ya kelele ya katikati ya usiku. Ujumbe wa katikati ya usiku utaweka Kanisa katika musimamo wake wa kweli wa mwanzo.

Kwa june 2002, kabla ya kuanza huduma hii, niliifanyia vibarua. Nilifanya ukurasa moja kwa ajili ya mkataba na ingine kwa ajili ya kanuni ya utaratibu ambapo nilieleza wazi kwamba sisi si wakatolika, wabatisti, wametodisti, wabranhamisti,… wala kinacho fanana na hao lakini [sisi ni] wakristo na kwa hiyo Biblia ni mkataba wetu pia kanuni ya ndani. Lakini wakapata bidii ya kunilazimu mkataba na kanuni ya utaratibu inayo lingana na ile ya vyama vya kipagani. Niliona ile kama matusi kwa vitu vitakatifu. Niliikataa! Je! Ni serikali au mamlaka ya dunia inayoweza kuniruhusu kusema yale Mungu alinituma niseme? Namna gani Yesu anaweza kumuomba Kaisari ruhusa kwa ajili ya huduma yake! Na namna gani twaweza kuomba vitu kama hivi na kisha, mpagani anaye nuka pombe atakuja kuchunguza kwa kuona kama mahubiri yangu inaambatana na nia ya wakuu wa kisiasa. Tunapojua kwamba Shetani ndiye mkuu wa dunia hii, namna gani anaweza kuniruhusu juu ya uwanja wake? Namna gani Elia anaweza kuomba kukubaliwa na Ahaba pamoja na Yezebeli? Namna gani Yoane Mubatizaji anaweza kuomba kukubaliwa na Herodia? Kufanya hivyo, ni kusaliti Mungu na kujiondoa hapo kwa mpango wa wokovu. Mungu anikinge na mambo haya kwani ni Serikali inayo pashwa kutii Kanisa. Tangu zamani za kale, Mungu hakupenda Israeli itii utawala fulani wala mfalme! Hii ndio msingi wa mateso ya kwanza ya Kanisa.

Ijapokuwa wakati kanisa inafanya vibarua, inapokea ruhusa ya Serikali, siyo tu tendo la utiifu lakini ni agano. Ni kama Amerika na Uingereza. Ni kama Suria inasahihi mapatano pamoja na Irak ili asaidiwe wakati atakapo shambuliwa na Israeli. Munaona? [Na tarehe 18 desemba 2005, wakati wa mahubiri ya wandugu mbele ya hekalu kubwa sana ya kibranhamisti iliyo huko Yopougon-Koweït, hao wabranhamisti walikimbilia polisi, munaona? Ninaona vibaya William Branham anapoita polisi ili wawapige wahubiri walio mbele ya Branham hekalu wala Yesu anapo waita maaskari warumi juu ya… lakini waaskari, makutano, watumishi… walikuwa kwa kazi ya wafarisayo na wasadukayo. Na ninawaambia tena mara ingine: kama mutahubiri mbele ya mahekalu, ningependa zaidi ziwe zile za wabranhamisti! Oh, niliambiwa kwamba waliimba kwa sauti kubwa kwa kusonga sauti ya wandugu lakini kimiujiza, sauti ya wandugu, niseme iliungana na sauti ya wamalaika, ikavuka ile kelele kubwa ya vyombo ambavyo viliweza kufananishwa na toleo la Bob Marley].

Ijapo, ni daima serikali inayochokoza Kanisa. Ni kama Herode ndiye anauliza Yesu kwa mamlaka gani anakuwa pale kwa kuhubiri! Munaona? Na siku moja, kaizari Constantin akaomba baraka juu ya mausoleum ya kumi na tatu aliyoijengesha kando ya zile kumi na mbili nyingine zilizo itwa kwa majina za mitume kumi na mbili. Na wakati wa sherehe ya kubariki mausoleum hiyo, muhubiri alipo kuwa akihubiri, Kaizari Constantin akasimama na akaamuru muhubiri asimamishe mazungumzo yake na abariki kwa upesi mnara. Munaona? Pale alikuwa amekubali wazi kwamba Serikali ilikuwa juu sana kuliko Kanisa. Alitaka kusema kwamba dunia ni juu ya mbingu na hapo mamlaka ya Kaisari ni juu ya mamlaka ya Mungu. Lakini hapo, alianguka vibaya kwani manabii waliotumwa na Mungu kwa kuonyesha watu ukuu wa Mungu juu ya Kaisari walikuwa duniani… [*Kusanyiko linasema: "Amina!"*].

Kwa Agosti 257, amri moja kutoka Roma ya upagani ikatangazwa kwa maneno haya: *"Aminieni kinacho wapendeza ninyi kwa namna ya upekee lakini kama wana-inchi, mujiweke kwa utaratibu wa shurti za nchi na musiunde aina ya Serikali ndani ya Serikali"*. Ambacho kilianguka katika masikio ya viziwi na ndiyo iliweza kuwa msingi wa mateso iliyochukua ma milioni za wakristo walio fahamu vizuri Waroma 13 kuliko ninyi. Munaona? Tunafanya vitambulisho vyetu, tunalipa kodi zetu, mea anaunganisha ndoa zetu, ni sehemu ya Kaisari. Munaona? Lakini kitu moja ambacho hatuwezi kufanya, ni kupatia serikali mamlaka juu ya kanisa au kubandika kanisa letu juu ya Serikali. Makanisa za shetani zinatii Serikali, sisi pia tunatii Biblia. Kama munatupenda sisi, mutuache hivyo! Kama tunapaswa kutii kwani ni Mungu anaye weka kila mwenyi mamlaka, wayahudi na Musa wangelibaki Misri wakati Farao alikataa. Na Danieli na wenzake wangeanguka kifudifudi mbele ya sanamu ya zahabu ya Nebukadneza! Nyinyi ni wana wa shetani, muna tabia ya kuanguka kifudifudi mbele yake na ninawasihi musijaribu kutuunga kwa uchawi yenu. Mbalimbali na Biblia, siwezi kuleta utambulisho ingine, picha tofauti na ile ya Kanisa ya Paulo, Petro, Wycliff, Lutheri, Kalvini, Wesley,… Kanisa haiwezi kuingizwa ndani ya Serikali. Kanisa Haiwezi kutawaliwa. Kati ya Kanisa na Serikali, kama kuna anayepaswa kutii mwingine, ni Serikali. Wakristo wa kwanza waliitambua vizuri. Hata wakatolika wanaijua vizuri kwa sababu kwa miaka nyingi, wapapa walitenga wafalme. Kwa mfano: kwa desemba 1301, papa Benoit VIII, katika maandiko yake iitwayo *Ausculta Fili* anakubali ukuu wa mamlaka ya kiroho juu ya mamlaka ya rahiya na ya muda. Wakatolika waliriti musimamo huo toka wakristo wa kwanza kabla warudi katika potopoto yao. Munaona? Siyo mawaziri na bunge vipofu wanao nuka uzinifu, pombe na uharibifu ambao watanisukuma. Ni kwenu kuwapa nafasi za heshima katika mikutano zenu! Ninajua faida ya Biblia ninayo shika ndio maana sina heshima kwa hizo katiba zenyi kupeperushwa ambazo hazita koma hata kidogo kurekebishwa. Ossius de Cordue, muhubiri mzee wa Uhispania akahamakia kaizari wa Roma kwa maneno haya: *" Huna ruhusa ya kujiingiza katika mambo ya dini! Mungu alikupa tu mamlaka juu ya nchi. Ni kwetu unalazimishwa kusikiliza somo, kwa mambo yanayo husu imani "*.

Na muhubiri mkuu Ambrwaze akalazimu kaizari Theodoze kukiri zambi hazarani kama watu wote, akimwambia hivi: *"Kaizari ni katika Kanisa, yeye si juu ya Kanisa. Musitumie Kristo lakini mumutumikie!*". Yoane Chrysostome akapaza sauti: *"Mamlaka ya Kanisa inapita sana kwa faida mamlaka ya rahia kama mbingu ilivyo juu sana kuliko dunia"*. Wakati siku moja kaizari Kostantino alisema: *"nyinyi ni mitume wa ndani lakini mimi ni mtume wa nje"*, majibu ikasikika mbele yake:

"Haiwezekani kuwa Kaisari na mkristo yote pamoja ". Ijapo leo, angeshangiliwa. Tunahubiri Injili ya zamani, sisi ni Kanisa ya kale. Na sisi ni juu ya dunia ya Mungu. Hatuna uriti pamoja na Kaisari. Kama Israeli, Kanisa ya kweli inashika kila mara msimamo kamili juu ya mamlaka ya muda. *"Kwa Kaisari yaliyo ya Kaisari; kwa Mungu yaliyo ya Mungu"*. Ni amri ya uungu na ninaitamka kwa jina la Yesu-Kristo kwa mamlaka ya huduma hii. Kuizuia, ni zambi.

Mimi siko kwa kazi kwani niliona uvuguvugu Kanisani wala kwa sababu nimegundua kweli moja ambayo wengine hawana, lakini ninaifanya sawa sawa na mwito wa tarehe 24 aprili 1993 na utumishi ambao sasa ni katikati yenu. Na kwa msingi wa Math.25:6, sijifanyi kile ambacho mimi siko. Na tangu sasa ninaweza kusema kwamba kelele imeletwa. Kama wewe ni nabii, mtume, mchungaji, injilisti, mwalimu, kwa unyenyekevu unalazimishwa kufwata nyuma ya hayo. Kama shabaa yako ni mbinguni, ni hiyo unalazimishwa kufanya.

Kumbuka kwamba kuna ishara za nje na ishara za ndani. Tetemeko za nchi, vita, kurudi kwa Israeli katika nchi yake,… ni alama za nje kwa dunia lakini Baragumu, nyota saba, kufunguliwa kwa mihuri (Ufu.6), ngurumo saba (Ufu.10:4), Kelele ya katikati ya usiku,… ni alama za siri za Bwana Arusi kwa Bibi Arusi. Dunia maana yake wakatolika, wabatisti, kusanyiko za miungu, wapentekoste, wa uamsho,… haiwahusu na hawaijui. Biblia inasema kwamba kwa makesha ya kuchukuliwa, kutakuwa Kelele moja itakayo amsha mabikira walio lala na itakayo peleka hata kwa kuchukuliwa na ni kwa hiyo ndipo tuko tukitazamia.

Nilisikia watu wakinenea Math.25:6 na sasa ni historia. Inakuwa kwa wakati uliyo pita: kelele ya katikati ya usiku imepiga. Munaona? Kila mtoto wa Mungu anafahamu kile ambacho Mungu iko akifanya na Kanisa ya Kweli inatembea sawa sawa na ahadi na unabii za Biblia. Kwani kama leo katika mwaka 2003, uamsho ikatokea ghafla katika kanisa fulani, inaweza kuwa vizuri lakini hiyo siyo uamsho ya Kanisa kwani, Biblia haisemi kwamba itakuwa bikira mmoja ndiye atakaye amka na kuamsha wengine lakini ni Kelele itakayo fanya kazi ile, ni Roho ya unabii inayo isema. Ombi letu ni kwamba Mungu anyanyue pale watu wanaofaa na pesa inayofaa kwani inalazimu kutafsiri ujumbe huu katika kiingereza, kijerumani, kiswahili, kihispania, kiportugal, kichina, kijapania,… Sawa sawa tunavyoona katika Biblia: Barua kwa wakorinto, kwa waroma, kwa wafilipi, Kwa Timoteo,… na leo wanaitumia duniani kote, ndivyo itakavyo kuwa kwa ujumbe huu ninayo wahubiri hapa. Jambo moja ya kufanya, ni kuitafsiri katika lugha nyingine. Munaelewa? Lakini kuhusu kuihubiri, Roho mtakatifu ataiambatanisha sawa sawa na kila nchi kwani manabii wa uwongo wa Zimbabwe siyo wale wa Afrika ya kati! Shirikisho ya makanisa za Portugal haiitwi CNEPE-CI! Askofu mkuu wa Paris haitwi Bernard Agré! Munaona? Hawatataja tena muhubiri Kacou Filipo lakini watataja Kelele ya Katikati ya usiku au ujumbe wa wakati! Kwa wakati ule ule mahubiri haya yatagawanywa popote!

Nilisema pia kwamba, watu walio katika nchi za kigeni, wanapo sukumwa na Roho, watarudi katika nji zao kwa kutangaza Kweli hii! Nyota zilizo tayarishwa kwa hali na wakati zitapandishwa huko na huko duniani. Zamiri ya wateule itaamshwa na watashika musimamo ngumu kinyume ya mamlaka yote ya dunia kama vile kwa mwanzo wa Kanisa. Tayari Tumefikia pale, yote inafwatana sasa na Roho ya Mungu ambayo iko ikiipanga kwa usawa huko na huko duniani. Basi kutakuwa hapo mawindo ya mtu na kukomesha "dini" kama hii ambayo wataiona kuwa ya uasi sana. Ni tendo la mwisho la unabii la Kanisa ya mataifa. Hiyo itaongoza kwa uamsho na kwa kuchukuliwa. Ni kwa unyenyekevu na kutambua tu kwa mwana wa Mungu ndipo huduma kama hii itastahili angalisho kwani Biblia inasema kwamba Ufalme wa Mungu hauje kwa namna ya kuonekana kwa macho. Basi aliye na masikio ya kusikia asikie!...

Kwa kumaliza, ningependa kusema kwamba wakati wote Mungu alipo patia Kanisa amani, Kanisa ilijiachilia kwa upungufu. Na kwa mfano kusema kuhusu ndoa,… kwanza kwa karne ya nne, Roma na Kanisa wakatambua kutoa mali kuwa alama ya ndoa. Hapo, ndoa ilitofautishwa na usuria kwa kutoa mali. Hakukuwa sherehe ya serikali wala ya kidini. Kisha serikali ikaanza kukamata atua pamoja na ile wanayoidai kuwa sherehe ya serikali, wanasema kwamba ni kutoa ndoa wazi wazi; sherehe iliyo pambwa na mkutano wa Roma kwa mwaka 721 pamoja na wasimamizi wanaume, wanawake na washuhuda kwa burudiko la kipagani iliyofatishwa na maandamano mitaani. Yote ile kwa roho ya kushindana na Kanisa. Kanisa, mbele ya hiyo sifa, ikaweka pia sherehe iitwayo ya baraka ambayo ilipiganishwa na wahubiri wasujaa kwani, walisema kwamba, ndoa yote inapo kuwa mapenzi iliyo ruhusiwa na Mungu na sasa kama ni vema kubaki pasipo kuoa kama anavyosema Paulo, hapo, sherehe ya ndoa hailazimishwi kuja hata Kanisani. Na toka kesho baadae nyuma ya mkutano wa Trente, nchi zikajitwalia mamlaka ya sherehe ya Ndoa wakionyesha kwamba ndoa ni kwanza mkataba wa serikali kabla ya kuwa sakramenti kawaida ya dini.

Kwa hivyo, nyuma ya kulipa mali kwa kuoa, wapagani walikuwa na sherehe ya serikali lakini wakristo hawakuwa nayo hata moja. Munaona? Kanisa na serikali hawakubaliani hata kidogo. Juu ya kanuni za ndoa, haki za bibi na bwana arusi au kusudi za kuachana, Kanisa na serikali hawakubaliani kamwe. Jambo lingine; Serikali inasema kwamba kama mtumwa akiomba kwa ndoa binti aliye huru, lazima mtumwa huyu auawe. Kanisa linasema kwamba mtumwa anaweza kuoa binti ya bwana wake kama binti huyo anakubali. Munaona? Hizo sherehe za sasa za serikali zinazo tangulia sherehe ya kidini tunazo ziona zilianza tokea karne ya XVIII zilizo anzishwa huko Ufaransa kwa sheria ya *"18 germinal"* na ni tu mtego wa Shetani, mamlaka yake ya serikali na makanisa zake kinyume ya Kanisa la kweli. Kanisa, katika historia, haikutambua kamwe ndoa ya serikali iliyo jengwa juu ya mamlaka ingine mbali mbali na Biblia. Mamlaka hiyo inapingana na Biblia na haikome kurekebishwa na yao yenyewe, kwa wakati wote, Kanisa haikuikubali. Sitaje makanisa lakini Kanisa.

Ni tofauti! Munaona? Kwenda kwa ofisi za mea na baada ya kutoka huko munakuja Kanisani, ni mtego wa Shetani na dunia nzima inashangilia nyuma ya mambo haya. Hapo Kanisa inatii Serikali. Na kusahihi hiyo mamlaka ingine ya ndoa ni kama kutolea miungu za warumi sadaka na kutia Kanisa chini ya Serikali. Munaona? Sawa sawa Serikali haina heshima kwa Kanisa, ndivyo sina heshima hata kidogo kwa Serikali na ndoa yake ya upagani. Kanisa ni mimi na nitafanya [yote] ili ipate kuheshimiwa. [*Kanisa inasema: Amina!!*]. Basi Kanisa irudilie msimamo wake wa kwanza!
[Kanisa inaimba: *Injili ya kale*].

MAWASILIANO: Ndugu Filipo:+ 225-0252-0252 E-mail: kacou.philippe@yahoo.fr
Upate mahubiri katika site ya: www.matth25v6.org